## HUDUMA YA USHAURI

TEMESA kupitia Idara ya Ushauri inatoa huduma za aina kuu mbili;

1. Huduma za ushauri wa kitaalamu (Consultancy services)
2. Huduma za ushauri wa kiufundi (Technical advice).



Jengo la Ofisi ya Bodi ya Mfuko wa Barabara lililopo maeneo ya Njedengwa, Manispaa ya Dodoma.TEMESA walishiriki kwenye mradi huu kama washauri upande wa mifumo ya Umeme, Viyoyozi, Lifti na TEHAMA.

**TEMESA** imepewa na Serikali jukumu la kutoa ushauri wakitaalamu na kiufundi kwa Serikali na watu binafsi katika fani ya kihandisi katika Nyanja za TEHAMA, Umeme na Mitambo.
Idara ya Ushauri inafanya kazi zote za Serikali na watu binafsi zinazohitaji ufundi na utaalamu wa kihandisi katika nyanja za:-
Katika kutekeleza kazi hizo, TEMESA inafanya shughuli zifuatazo;

### A. Huduma za ushauri wa kitaalaamu (consultancy services).

1. Kuaanda michoro na kusimamia kazi zilizoandaliwa.

2. Kuaandaa zabuni kwa ajili ya taratibu za kupata wakandarasi.

3. Kuandaa mikataba kati ya Mshitiri na Mkandarasi au Mkandarasi na wakandarasi wadogo.

4. Tunaandaa misawazo ya kiufundi (technical specifications).

### 2. Huduma za Ushauri wa Kiufundi (Technical advice).

Katika kutekeleza kazi ya kutoa huduma za Ushauri wa kiufundi (Technical advice) Idara ya Ushauri inafanya shughuli zifuatazo;

1.Kuandaa msawazo "specification" ya mitambo na magari.

2. Kushauri serikali pamoja na taasisi zake juu ya ununuzi wa mitambo na magari.

3. Kukagua na kusimamia ufungaji na ukarabati wa mitambo na magari.

4. Kukagua mitambo ya umeme katika majengo ya serikali na taasisi zake.

5. Kufanya vipimo stahiki vya umeme kwa niaba ya wateja pale inapohitajika na kushauri Tanesco.

6. Usajili na ufutaji wa magari na mitambo ya serikali.